



## UKWELI JUU YA ROHO MTAKATIFU

(Truth About the Holy Ghost)

### UTANGULIZI

"Mungu ni Roho' (Yohana 4:24) Roho wa Mungu anajulikana kama Roho Mtakatifu. Ni Roho wa Mungu aliye umba vitu vyote vilivyomo katika ulimwengu. Roho Huyu ndiye aliyemfanya mariamu kutya mama wa Yesu. Roho Mtakatifu katika Yesu ndiye aliyemfanya Yesu Mungu na kumfufua katika wafu.

Roho wa Mungu anataka kukaa ndani ya kila mmoja. Anata.ka kufanya makaoyakendani yako. (1 Wakorintho 6:19) Mambo haya ndiyo yanayo fanyika mtu akiisha pokea Roho mtakatifu,, Roho wa Kristo huingia na kukaa ndani yako.

### JE, NI NANI AWEZAYE KUPOKEA ROHO MTAKATIFU?

Mambo haya yameahidiwa watu wote kila mahali (Matendo ya Mitume 2:39). Jambo la kufanya ni kutubu, kubatizwa katika jina

la Yesu, na kumuuliza Mungu Roho Mtakatifu (Matendo 2:38), (Luka 11:13). Ni mapenzi ya Mungu kukujaza Roho Mtakatifu, Muulize, weka tumaini lako Kwake, naye atafanya hivyo.

Katika Agano la Kale, Mungu alisema kwamba siku za rnwisho atawajaza watu wote na Roho Mtakatifu (Yoeli 2:28). Yohana Mbatizaji alisema kwamba Yesu Ndiye atakaye batiza watu na Roho Mtakatifu, (Madiayo 3:11) Yesu alieleza watu wake kwamba atawaacha lakini kwamba atawarudia tena katika njia ya Roho Mtakatifu (Yohana 14). "Kama ye yote anayo kiu, aje kwangu na anywe. Maandishi Takatifu inasema kwamba mito ya uzima itafurika kwenye moyo wa ye yote awekaye imani yake kwangu. Yesu alisema mambo haya juu ya-Roho Mtakatifu atakaye kuja kwa wote watakao weka imani yao kwake. Roho Mtakatifu alikuwa hajapeanwa. Yesu alikuwa bado hajainuliwa mahali penye utukufu. (Yohana 7:37 - 39)

#### UKWEU JUU YA ROHO MTAKATIFU UNAENDELEA:

JE, NITAFAHAMU NAMNA GANI KWAMBA NINAYE ROHO  
MTAKATIFU?

Utanena kwenye lugha nyingine ambayo Roho mtakatifu atakupa baada ya kumpokea. Kwa mara ya kwanza Roho Mtakatifu kupeanwa katika Matendo 2:4, Biblia inasema, "Wote wakaanza kunena kwa lugha nyingine ambayo Roho mtakatifu aliwawezesha kunena."

Mungu alinena kupitia nabii Isaya kwamba mambo haya

yatafanyika. 'Bali kwa midomo ya watu wageni, na lugha nyingine Mungu atanena na watu Wake.

(Isaya 28:11) Yesu akasema ya kwamba watu wote watakao weka imani yao kwake, watanena kwa lugha hata ile hawakujifunza (Marko 16:17).

Petro alifahamu ya kwamba watu wa Mataifa walipokea Roho Mtakatifu kwa sababu aliwasikia wakinena kwa lugha nyingine kwenye nyumbe ya Komelio (Matendo ya Mitume 10:46). Katika matendo ya Mitume 19:6, Wakati Paulo aliweka mikono yake juu yao, "Roho Mtakatifu aliwashukia. Wakaanzakunena kwa lughanyingine na kumtukuza Mungu." Hii inazungumza juu ya wafuasi wa Efeso. Watu wa Mungu hata leo hunena kwa lugha wanapo pokea Roho Mtakatifu.

### **KUMALIZA:**

Yesu akamwambia Nikodamu, "Amin. amin nakwambia mtu asipozaliwa kwa maji na Roho wa Mungu, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu (Yohana 3:5). Kule kukataliwa kuingia kwenye taifa takatifu la Mungu nikusema ya kwamba, utaadhibiwa milele na milele kwa ajili ya dhambi zako.

Mungu anataka uingie katika taifa lake takatifu. Karna utatubu, kubabzwa katika Jina lake, na kupokea Roho Mtakatifu basi utaingia. Kwa hivyo, ingia kwenye uzima na furaha na amani ambayo ni ya milele na milele.